# OFISI YA RAIS TAMISEMI

## (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)

## MKOA WA KIGOMA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU

KASULU DISTRICT COUNCIL

**KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA MWEZI OKTOBA 2021/2022 TAREHE 17/12/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA KASULU.**


***Imeandaliwa Na:***

**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji**

**Halmashauri ya Wilaya**

**S. L. P 97**

**KASULU.**

***www.kasuludc.go.tz***




CamScanner

**AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 17/12/2021.**

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha Agenda za kikao cha tarehe 07/12 /2021.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 27.10.2021.
4. Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 27.10.2021.
5. Taarifa ya Fedha Mapato na Matumizi Mwezi Oktoba 2021.
6. Maombi ya kufuta hasara ya upotevu wa fedha shs 2,880,000
7. Taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya UVICO19 kiasi cha shilingi 2,455,178,634.67 kwaajili ya ujenzi wa vymba vya Madarsa 90,shule za sekondari, posho za chanjo za Covid,ufuatiliaji wa tathimini, ujenzi wa nyumba ya watumishi,uhamasishaji wa chanjo na ujenzi wa kituo cha matibabu.
8. Mengineyo
9. Kufunga kikao



CamScanner

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA ROBO MWEZI OCTOBA 2021/2022 TAREHE 07/12/2021.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| NA | JINA KAMILI | KATA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Eliya C. Kagoma | Diwani Kata ya Kitanga | Mwenyekiti Halmashauri |
| 2. | Mhe. Poteza L. Kilali | Diwani Kata ya Makere | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Asia Kasebo | Diwani Viti Maalumu | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Fabiano Doragi | Diwani Kata ya Rusesa | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bryson Milinga | Diwani Kata ya Kwaga | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mwasi Mchunga | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Jonas Kaja | Diwani kata ya Rungwe Mpya | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Sabas Matabula | Diwani kata ya Kitagata | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

1.Mhe. Agustino Vuma Hole, Mbunge Jimbo la Kasulu Vijijini – kwa taarifa



CamScanner

**WATAALAMU WALIOHUDHURIA**

| NA | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Less Majala | Mkurugenzi Mtendaji (W) |
| 2. | Michae Magesa | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 3. | Cosmas Msema | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 4. | Eias Mtakama | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 5. | Joseph Maiga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 6. | Gwamaka Panja | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 7. | Jeconia J. N | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi. |
| 9. | Pelimina Msuta | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. |
| 10. | Peter Kitogwe | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 12. | Bahati Onesmo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 13. | Mohamed Omary | Afisa Nyuki |
| 14 | Audax Kamugisha | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 15 | Dr. | Kwa niaba ya Mganga Mkuu |
| 16 | Kilatu J.W | Mkuu wa Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji. |
| 17 | Revocatus Mwombeki | Afisa Biashara |
| 18 | Almachus Njungani | Mratibu wa TASAF |
| 20 | Chacha Matiko | Mhasibu wa Mapato |
| 21 | Atanas Msuts | Kaimu Mhandisi wa Halmashauri |
| 22 | Nyiganda C.Nyiganda | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na ushirika |
| 23. | Vanica Ndelekwa | Mkuu wa Idara ya Usafi na mazingira |

**SEKRETARIETI.**

1. Fiona E. Sephania.
2. Hildephonce Mchunguzi

**HWK/ FUM /AG. Na/24/2020/2021 KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwaomba kuchangia maoni yao na ushauri katika Agenda zitakazojadiliwa. Baada ya kusema hayo alifungua kikao mnamo saa 4:00 Asubuhi.

**HWK/ FUM/AG.NA/25/2021/2022.KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 07.12.2021**

Agenda tisa (9) ziliwasilishwa, wajumbe walizipokea na kuridhia zijadiliwe kwenye kikao hicho Kama ifuatavyo .

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha Agenda za kikao cha tarehe 07/12 /2021.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 27.10.2021.
4. Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 27.10.2021.
5. Taarifa ya Fedha Mapato na Matumizi Mwezi Oktoba 2021.
6. Maombi ya kufuta hasara ya upotevu wa fedha shs 2,880,000
7. Taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya UVICO19 kiasi cha shilingi 2,455,178,634.67 kwaajili ya ujenzi wa vymba vya Madarsa 90,shule za sekondari, posho za chanjo za Covid,ufuatiliaji wa tathimini, ujenzi wa nyumba ya watumishi,uhamasishaji wa chanjo na ujenzi wa kituo cha matibabu.
8. Mengineyo
9. Kufunga kikao

**HWK/ FUM/AG.NA/26/2021/2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 27.10.2021.**

Muhtasari wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa tarehe 27.10.2021 ulisomwa; wajumbe wa kikao waliupokea na kuuridhia na kisha ulisainiwa kuwa kumbukumbu ya kikao cha tarehe husika.

**HWK/FUM/AG.NA/27/2021/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 27.10.2021**

Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 27.10.2021 iliwasilishwa kwa wajumbe wa kikao kisha waliipokea, kuijadili na kuazimia kama ifuatavyo -;

- Iliazimiwa kuwa magari ya kubeba wagonjwa ya kituo cha Afya Nyenge Rusesa yawe yametengenezwa na kuendelea kufanya kazi katika vituo taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kikao kijacho cha kamati. Aidha ilisistizwa kuwa baada ya vifaa vya kutngenzeza magari vilivyoagizwa kufika magari yote yatengenezwe na gari la Idara ya Utumishi na Utawala lipewe kipaumbele katika magari yatakayotengenezwa kwani limepaki kwa muda mrefu.



CamScanner

- Iliazimiwa kuwa kikao kijacho cha kamati Mhandisi awasilishe taarifa ya gharama za utengenezaji wa jenereta la Halmashauri awasiliane na mafundi wengine kutoka nje ya halmashauri wasaidie kufanya tadhimini hiyo taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kikao kijacho cha kamati.

- kuazimia kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri aandike andiko kwenda kwa Wazairi wa TAMISEMI kwa ajili ya kumkumbusha juu ya ahadi aliyoahidi ya kutoa mwongozo mpya wa posho za vikao za madiwani na Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala apeleke andiko hilo kwa Waziri kabla ya tarehe 25.12.2021.

**HWK/FUM/AG.NA/28/2021/2022. TAARIFA YA FEDHA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI OCTOBA 2021**

Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Mwezi Octoba 2021 iliwasilishwa na Mweka Hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji kama ifutavyo-;

Halmashauri ya Wilaya Kasulu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imekadiria kukusanya jumla ya Tsh. 30,954,065,930.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya miradi ya maendeleo ambapo Tsh. 14,855,654,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara, Tshs.7,340,651,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa Idara zinazopokea ruzuku,Tshs 300,000,000.00 ni ada ya Huduma, Tshs 350,000,000.00 ni CHF na NHIF, Tshs 123,000,000.00 ni mchango wa ada za kidato cha tano na sita,Tshs.2,119,312,430.00 ni mapato ya vyanzo vya Halmashauri na Tsh.12,471,448,500 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mwezi Octoba 2021 mapato halisi ya Halmshauri ni kiasi cha Tsh.2,104,888,245.7 sawa na asilimia kumi na tisa (19) ya mapato kwa mwaka 2021/2022.

Aidha mwezi Oktoba Halmashauri imefanya matumizi ya kiasi cha shilingi 1,593,418,599.4. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea, kushauri na kuazimia kuwa

Wajumbe walisisitiza Menejimenti kujipanga vizuri katika kukusanya mapato ili na kusimamia vyanzo vya zamani, vipya na kubuni vyanzo vipya vya mapato.

**HWK FUM /AG.NA/30/2021/2022. TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA UVICO19 KIASI CHA SHILINGI 2,455,178,634.67 KWAAJILI YA UJENZI WA VYMBA VYA MADARSA 90,SHULE ZA SEKONDARI, POSHO ZA CHANJO ZA COVID,UFUATILIAJI WA TATHIMINI, UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI,UHAMASISHAJI WA CHANJO NA UJENZI WA KITUO CHA MATIBABU.**

Taarifa ya Halamashaumari kupokezi ya fedha za miradi ya UVICO19 kiasi cha shilingi 2,455,178,634.67 kwaajili ya ujenzi wa vymba vya madarsa 90,shule za sekondari, posho za chanjo za COVID,ufuatiliaji wa tathimini, ujenzi wa nyumba ya watumishi,uhamasishaji wa chanjo na ujenzi wa kituo cha matibabu iliwasilishwa kwnye kikao kama ifuatavyo-;



CamScanner

Fedha kiasi cha 1,800,000,000/= kwaajili ya ujenzi wavyumba vya madarasa 90 shule za Sekondari19,shilingi 27,428,121.54 posho za chanjo,shilingi 6,514,747.00 ufatiliaji wa tadhimini,shilingi 90,000,000.00 ujenzi wa nyumba ya Watumishi 3 in 1 shilingi 31,251,075.51 uhamasishaji wa chanjo na shilingi 500,000,000.00 ujenzi wa kituo cha matibabu. Baada yakuwasilisha wajumbe walipokea taarifa na kujadili yafuatayo

Wajumbe walimpongeza Raisi wa Jamuhuri ya muungao wa tanzania kwa kutoa fedha za ujenzi wa madarasa kwani swala hili limekuwa ni mzigo mzito kwa wananchi hivyo amewatua mzigo mzito.

- Wajumbe walishuri kuwa fedha za ujenzi wa madarasa zisimamiwe vizuri na waliazimia kuwa vifaa vya kiwandani kama kunauwezekano viagizwe moja kwa moja kiwandani kwa kuwa tukiwatumia wazabuni wa hapa tutachelewa kufanya kazi kwa wakati na bei ya bidhaa itakuwa juu zaidi.
- Wajumbe wamesisitiza kuwa fedha zote tulizopokea zifanye kama hakuna kikwazo zianze kufanya kazi mara moja na zifanye kazi kulingana na maelekezo yaliyotolewa.
- Wajumbe wamesisitiza kuwa kamati za manunuzi na kamati za ujenzi katika miradi hii zishiikishwe kukamilifu katika kutekeleza na taratibu zote za matumizi ya fedha za serikali zifuatwe ili kuepuka hoja za wakauzi na kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali.
- Wakuu wa idara wote wakishirikiana na Waheshimiwa Madiwani wasimamie ujenzi huu kwa kushirikiana na kupeana taarifa ili kuweza kukamilisha kwa wakati.

**HWK/FUM/AG.NA/29/2020/2021: MAOMBI YA KUFUTA HASARA YA UPOTEVU WA FEDHA SHS 2,880,000.**

Maombi ya kufuta hasara ya upotevu wa fedha kiasi cha Tsh.2,880,000 kwa mkusanya mapato (RS) wa Kurugongo bwana aliyevamiwa na majambazi akiwa anatekeleza majukumu yake kwenye kituo cha kazi na kupigwa risasi iliwasilishwa na Mweka Hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji baada ya hukumu kutolewa nakala ya hukumu hiyo iliwasilishwa kwa wajumbe. Baada ya uwasilisha hiyo wajumbe walipokea na kujadili baada ya kujiridhisha waliridhia kuwa hasara hiyo ifutwe ili mkusanya mapato huyo aendelee na kazi.

**FUM /AG.NA/31/2021/2022. MENGINEYO:**

Katika agenda hii mjumbe aliwasilisha taarifa kuwa Wananchi wa Wilaya ya Uvinza wamevamia eneo la Halamashauri ya Wilaya Kasulu katika kata ya Rusesa na kuweka mipaka hivyo menejimenti ione namna ya kutatua na kushughulikia tatizo hilo ikiwemo kwenda kuona eneo hilo lililovamiwa



CamScanner

**FUM /AG.NA/32/2021/2022. KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa majadiliano mazuri alisistiza kufanyia kazi maagizo na maazimio yote yaliyo azimiwa kwenye kikao aidha alisistiza kuwa menejimenti kufanyia kazi maoni na maagizo ya mkaguzi wa ndani juu ya hoja zilizohojiwa na Mkaguzi wa ndani. Baada ya kusema hayo, alifunga kikao saa 09:00 Alasiri.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA:**

| | |
|---|---|
| JESSI J. MAJOLA | ELIYA C. KAGOMA |
| Katibu | Mwenyekiti |
| ……………………… | E. Charles |
| Saini | Saini |
| Tarehe 17/12/2021 | Tarehe 17/12/2022 |